

Mfuko
wa Kujikimu
ISHI VIZURI ...UNASTAHILI



Mfuko wa Jikimu ni mfuko wenye lengo la kutoa gawio na kukuza mtaji kwa wawekezaji wake kwa muda wa kati na muda mrefu. Mfuko unawekeza katika hisa na masoko ya fedha.

Lini nianze kuwekeza fedha zangu?

Anza mapema uwezavyo kununua vipande vya Mfuko wa Kujikimu, kwa sababu utakavyoanza kuwekeza mapema ndivyo unavyotoa muda mrefu wa fedha kuwekezwa na kukupa faida zaidi. Kila mwaka kiasi kitakachoongezeka (faida) kitazalisha faida nyingine katika miaka itakayofuata faida inazidi kuongezeka na huku mtaji nao ukiongezeka kadri miaka inavyoongezeka. (Compounding Interest / Faida Jumuishi)

Nani anayefaa kuwekeza katika mfuko wa Kujikimu.

- Mtanzania mkazi na asiye mkazi.
- Vikundi, Kampuni, Asasi, Taasisi na Mashirika mbalimbali.

Kwa nini Mfuko wa Kujikimu?

- **Gawio:** Mara moja au mara nne kwa mwaka
- **Usalama:** Uwekezaji mseto katika hisa na dhamana mbalimbali
- **Faida:** Licha ya kupata gawio mara kwa mara pia mtaji wako utaongezeka.
- **Ukwasi:** Urahisi wa kupata sehemu au fedha zako zote pale utakapozihitaji.
- **Uwazi:** Thamani ya kipande inatolewa kila siku ya kazi.
- **Gharama:** Mfuko unaendeshwa kwa gharama nafuu.
- **Kuratibiwa:** Mfuko unaratibiwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana.

Aina za uwekezaji:

1. Mpango wa gawio

Mwekezaji akiwekeza milioni moja atapata gawio mara moja kwa mwaka na akiwekeza milioni mbili au Zaidi atapata gawio mara nne kwa mwaka.

2. Mpango wa kukuza mtaji

Mwekezaji anaweza kuamua kutochukua gawio lake ili kukuza mtaji wake, hadi siku atakapo zihitaji.

Mfano

Jedwali hapa chini linaonyesha mwekezaji aliyewekeza shilingi milioni 50 katika mpango wa gawio la mara nne kwa mwaka, amekua akipata faida ya asilimia 3 hadi 4 kila baada ya miezi mitatu tangu kuanzishwa.

Kiasi	Ukuaji robo mwaka	Gawio la robo mwaka	Gawio kwa Mwaka
50,000,000	4%	2,000,000	8,000,000
50,000,000	3%	1,500,000	6,000,000

Jedwali linaonyesha kiwango cha juu cha gawio ni asilimia 16 kwa mwaka, yaani asilimia 4 kila robo mwaka. Pale ambapo mfuko utakuwa umekuwa zaidi ya asilimia zilizotajwa ongezeko hilo litaongezwa kwenye mtaji wa mwekezaji.

**Wekeza Kwa
Njia Ya Simu**

***150*82#**

**KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS, S.L.P 14825, GHOROFA YA PILI JENGO LA SUKARI,
MTAA WA SOKOINE NA OHIO, DAR ES SALAAM**

Simu: +255 22 2122501 | Nukushi: +255 22 2137593 | Wakala: UTT MICROFINANCE • MATAWI YOTE YA BENKI YA CROB NCHINI • MADALALI WOTE
WA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM. | Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz | Tovuti: www.uttamis.co.tz |

Namba Za Bure +255 754 800 544 na +255 754 800 455 (VODA) +255 715 800 544 na +255 715 800 455 (TIGO) +255 782 800 455 (AIRTEL)

Tahadhari: Thamani ya kipande inaweza kuongezeka au kupungua

